



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII



CHUO CHA MAFUNZO YA MISITU NA VIWANDA VYA MISITU, MAFINGA

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MISITU NA UCHAKATAJI MAZAO YA MISITU
NGAZI YA VET LEVEL I - III KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu kilichopo Mafinga - Iringa anatangaza nafasi za maombi ya kujiunga na mafunzo kwa fani za Uhudumu misitu na Uchakataji wa mazao ya misitu ngazi ya VET Level I - III kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

A. Fani zinazotolewa:

- i. Astashahada ya Uhudumu misitu - Miaka miwili (2);
- ii. Astashahada ya Uchakataji wa Mazao ya Misitu - Miaka miwili; (2);

B. Sifa za mwombaji:

i. Astashahada ya Uhudumu misitu

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu wa angalau alama **D** katika masomo mawili yasiyo ya dini.

ii. Astashahada ya Uchakataji wa Mazao ya Misitu

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu wa angalau alama **D** ya somo moja kati ya Biolojia au Kemia

C. Ada ya mafunzo

Ada kwa mwaka wa kwanza itakuwa **Sh. 560,000/=** na inaweza kulipwa katika awamu mbili, yaani kila awamu **Sh. 280,000/=**.

D. Jinsi ya kutuma maombi

- i. Maombi yatumwe kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi; <https://saris.maliasili.go.tz/Registration/28> au kwa kujaza fomu za maombi ya kujiunga na Chuo. Fomu zinapatikana kwenye tovuti ya Chuo <http://www.fwitic.ac.tz>
- ii. Gharama ya maombi ya kujiunga na chuo ni Tsh. 10,000.00 tu. Malipo yote yanafanyika kwa kutumia Control number inayoonekana kwenye kiunganishi. Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana nasi kwa simu namba 0763320102 au 0747203643.

Karibuni nyote